19. The Bookshop

19. The Bookshop

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA TISA kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.
The Bookshop ni riwaya iliyoandikwa na PENELOPE FITZGERALD inayohusu mwanamke aliyeona fursa ya kufungua duka la vitabu na kuifanyia kazi lakini anakutana na vikwazo vikubwa na biashara inakufa.

👉1
Mwaka 1959, Florence Green alikuwa hapati usingizi kwa usiku mzima. Alikuwa na mawazo mengi kuhusu jengo kuu alilotaka kununua ili kulifanya kuwa duka pekee la vitabu kwenye mji wa Hardborough.
Florence alikuwa ameachiwa urithi kidogo na mume wake aliyefariki na aliona anahitaji kuwa na njia ya kuingiza kipato zaidi.
Anaenda benki kwa ajili ya kuomba mkopo ambapo afisa wa benki anamhoji maswali mbalimbali. Kwanza anamtaka ajue lengo lake la kufungua biashara ni nini? Je anataka kutoa huduma ambayo watu wanahitaji? Anataka kutengeneza faida? Au anaingia tu kwenye biashara bila ya lengo au uelewa wowote?
Anamuuliza uzoefu alionao kwenye biashara ta vitabu ambapo Florence anamjibu mume wake alikuwa mshairi, japo hajajua kama kuna mabadiliko kwa sasa.
Afisa wa benki anamwambia kama mfanyabiashara lazima ajue kufuatilia hesabu za pesa ili pale pesa inayotoka inapokuwa kubwa kuliko inayoingia, ajue kuna hatari mbele.
Afisa huyo anamweleza japo kwa sasa mikopo haitolewi kirahisi, kuna uwezekano akapata.
Florence anamweleza kiasi kinachohitajika kununua nyumba ile kuu, afisa wa benki anamwambia ni kiasi kikubwa, ni bora asubiri maana bei itaendelea kushuka.
Mji wa Hardborough umekuwa unaendelea kudorora kadiri siku zinavyokwenda, usafiri wa reli umesitishwa na njia kuu ya usafiri ni ya maji kupitia boti ndogo ndogo.
Florence anarudi nyumbani kwa miguu huku akitembea kwenye mitaa ya mji huo.
Anakutana na bwana Raven ambaye huwa anafanya kazi ya kulisha wanyama.
Anamuita na wanasalimiana, anamuomba amsaidie kumshika farasi ambaye amekabwa na majani ili amsaidie aweze kula.
Raven anamwambia Florence anajua hawezi kuogopa hilo. Florence anamuuliza nini kimemfanya ajue hivyo? Raven anamjibu amesikia habari kwamba anataka kufungua duka la vitabu, hicho ni kiashiria kwamba yuko tayari kufanya vitu vya tofauti.
Wanamsaidia farasi yule na kisha Florence anaondoka huku akitafakari sana kauli ambayo Raven amemuambia.

👉2
Florence anakamilisha manunuzi ya jengo kuu na analifanyia marekebisho ili aweze kuhamia.
Jengo hilo lina miaka zaidi ya 500 na kumekuwa na habari kwamba huwa linatembelewa na mizimu inayotupa vitu nje.
Lina vyumba vya chini na juu, ambapo Florence anapanga awe anatunza vitabu vyumba vya juu.
Changamoto kubwa ni kwamba jengo hilo huwa linaingiza maji kunapokuwa na mafuriko na kwa kuwa liko ufukweni, huwa linakuwa na unyevu muda mrefu, kitu kitakachoathiri vitabu.
Florence analeta fundi wa kufanya marekebisho na kisha kuhamia.
Anaalikwa kwenye sherehe iliyoandaliwa na Mrs Gamart ambaye ametoka London kuja hapo Hardborough.
Hajazoea kualikwa sherehe za aina hiyo, anafika na mume wa Mrs Gamart ambaye ni Jenerali ndiye

anayeanza kuongea naye. Florence anajitambulisha ndiye anayepanga kufungua duka la vitabu. Wanaongea kwa muda na anaondoka.
Anakutana pia na kijana anayeitwa Milo ambaye pia anamuuliza kama kweli amejiandaa kwa biashara hiyo na kama mji huo una wasomaji wa vitabu. Florence anamjibu anaamini wapo na yeye Milo ni mmoja wao.
Baadaye Mrs Gamart anakuja kuongea na Florence anamuuliza kama ameshahamia kwenye jengo kuu, anamjibu ndiyo. Anamuuliza amehamiaje wakati halina matengenezo, anamjibu amefanya matengenezo.
Mrs Gamart anamwambia lengo la kumuita hapo ni kumweleza mpango walio nao, kwamba jengo hilo kuu, ambalo ndiyo kuu kuliko mengine ligeuzwe kuwa kituo cha sanaa na siyo duka la vitabu.
Anamwambia kuna jengo jingine liko wazi, anaweza kulitumia hilo kufungua duka la vitabu na jengi hilo kuu likawa la sanaa.
Mrs Gamart anampa Florence nafasi ya kusimamia kituo hicho cha sanaa.
Florence anamjibu kwamba alikuwa kwenye mapatano ya kununua jengo hilo kwa zaidi ya miezi sita na hakuna aliyemwambia hilo, anashangaa kusikia sasa.
Sherehe inaisha na Florence anaondoka akifikiria kama anaweza kufanya vyote kwa pamoja, duka la vitabu na kituo cha sanaa.
Mrs Gamart anabaki akifikiria kwamba Florence hajakubaliana na hilo na hivyo anafikiria watu anaowajua serikalini ambao wanaweza kusaidia kupitisha sheria ya kuhakikisha jengo hilo kuu linakuwa kituo cha sanaa.

👉3
Florence anafikiria pendekezo la Mrs Gamart kuhusu kituo cha sanaa na kumtembelea Mr Deben ambaye ana jengo lililo wazi.
Mr Deben anamwambia japo jengo lake litakuwa wazi, asitegemee sana kulipata.
Florence anafikiria kuhusu majengo mengine kwenye mji huo na hata nje ya mji.
Lakini baadaye anatafakari na kuamua kwamba hataondoka kwenye jengo hilo kuu, kama Mrs Gamart anataka akatafute jengo jingine la kuanzisha kituo cha sanaa.
Vitabu alivyokuwa ameagiza vinafika, anapata vijana wa skauti wanaomsaidia kuweka mashelfu na yeye anavipangilia vitabu kulingana na anavyoona vitawavutia wateja.
Anaongea na mhasibu atakayekuwa anamsaidia kupitia hesabu zake za biashara angalau mara moja kila mwezi.

👉4
Siku ya kufungua duka la vitabu inafika, Florence hajapanga kuwa na tukio kubwa la ufunguzi.
Mr Raven anamtembelea na kumueleza kwamba anahitaji kuwa na msaidizi, mtoto wa shule atakayemsaidia kwa masaa machache kwa siku.
Wakiwa hapo Wally kijana wa skauti anakuja na ujumbe kutoka kwa Mr Brundish, mmoja wa wakazi maarufu wa mji huo ambaye kwa muda amekuwa ndani kutokana na maradhi.
Florence anafungua ujumbe huo, ameandika kumpongeza kwa kufungua duka la vitabu maana mji huo haujawa na duka la vitabu kwa muda mrefu.
Anamwambia pia atashukuru kama akianzisha maktaba ya kuazimisha vitabu.
Florence anaona hakuwa amefikiria hilo, anaona ni fursa pia, ila tatizo ni nafasi yake ni ndogo.
Wiki ya kwanza ya kufungua duka mauzo yanakuwa makubwa kuliko alivyotegemea, watu mbalimbali wanakuja kununua vitabu.
Hata aliyemuomba awe anapitia hesabu zake za biashara, anashangazwa na ukubwa wa mauzo kwenye mwezi wa kwanza wa biashara.
Anamuuliza maswali mbalimbali kuhusu mali na madeni ya biashara, anagundua Florence hajui hesabu hizo. Anamwambia ni muhimu sana katika wakati wowote ule ajue hali ya kifedha ya biashara yake ikoje.
Anaanzisha huduma ya maktaba anbayo inafunguliwa mara moja kwa wiki, lakini anashindwa kwenda

nayo kwa muda mrefu kwani watu walikuwa wanataka kitabu cha aina moja na hivyo ikaishia kuwa lawama.
Anaahidi kurudisha huduma hiyo baada ya kuwa amejipanga.

👉5
Florence anaona wazi kwamba anahitaji msaidizi, hawezi kufanya kila kitu peke yake.
Anaulizia kwa watu na kuambiwa watoto wa Gipping wanaweza kumsaidia vizuri.
Christine mwenye miaka kumi anakuja kwa Florence na kumwambia yuko tayari kumsaidia, japo ni mdogo, anaonekana kujua mengi na kuwa tayari kwa kazi.
Anakuwa msaidizi wake na anamsaidia kwenye majukumu mengi.
Msimu wa sikukuu unafika na Florence anaona licha ya kuishi karibu na ufukwe, hajautembelea kwa muda mrefu. Anatembelea ufukwe na kukutana na watu mbalimbali. Wengi wanaomjua wanamuuliza lini huduma ya maktaba itarudi, anawaahidi muda si mrefu.
Mkaguzi wa hesabu anakuja tena na kukuta makosa ni mengi zaidi kwenye hesabu za biashara na kuna hasara kubwa. Florence anaonekana kutokuwa na uelewa kwenye mengi.
Milo anakuja dukani akitaka zawadi ya kitabu kwa ajili ya mke wake, Florence anamchagulia.
Milo anamuuliza Florence kama Mrs Gamart ameshamtembelea, anamjibu bado. Milo anamwambia lazima atakuja tu, maana huwa hakubali kushindwa jambo lake.
Milo anamuuliza kama anaingiza faida kwenye biashara hiyo, swali ambalo anashindwa kulijibu moja kwa moja.
Anamshauri kitabu kizuri cha kuweka ambacho kitauza sana.

👉6
Siku moja usiku Florence akiwa na Christine wanasikia sauti ya ajabu kwenye vyumba vya juu.
Wote wanakaa kijasiri na hawataki kuonesha kwamba wana hofu.
Sauti hiyo inaendelea kwa muda na wanashindwa kuvumilia.
Christine anamwambia huo ni mzimu umewatembelea na mama yale alishamwambia nyumba hiyo huwa inatembelewa na mizimu.
Baada ya dakika kumi sauti hizo zinatulia.
Kesho yake Christine anapokuja kazini anamwambia mama yake ameshauri mzimu ukija tena wapige magoti na kusali.
Florence anafikiria mengi, ikiwepo kama dhana ya mizimu ni ukweli au imani tu.
Milo anakuja tena dukani kwake na kumuuliza Florence kama ameshaagiza kitabu alichomshauri, kinachoitwa Lolita, anamjibu bado hajafanya maamuzi.
Anamuuliza nini kinamchelewesha, Florence anajibu amesikia wachambuzi wengi wakisema siyo kitabu kizuri.
Milo anamsisitiza afanye maamuzi na kukiagiza, kwani kitamsaidia sana pale mambo yatakapokuwa magumu.
Kauli hiyo ya mambo kuwa magumu anashangaa inajirudia mara kwa mara, maana hata Raven kuna mboga alimshauri awe nazo kwani zitamsaidia mambo yakiwa magumu.
Miezi 6 imepita tangu amefungua biashara, hesabu zake ziko vizuri, mtaji unaozunguka ni mkubwa na benki ana akiba.
Amekuwa akibana sana matumizi yake binafsi na ya biashara pia.

👉7
Florence amefungua tena huduma ya maktaba ya kukodi vitabu na sasa Christine anaisimamia vizuri, zile changamoto za awali zimepungua.
Siku moja Mrs Gamart anakuja kwenye duka la Florence, siku hiyo kulikuwa na wateja wengi wa kununua vitabu na wa kukodi pia.
Florence alitamani amhudumie mwenyewe lakini akawa amebanwa. Mrs Gamart akaenda kuhudumiwa na Christine, lakini wanashindwa kuelewana na anatoka akiwa na hasira.
Florence anamuuliza Christine nini kimetokea, anamjibu Mrs Gamart hakutaka kukaa foleni na

alichukua vitabu vya wenzake, alipomkatalia ndiyo wakagombana.
Florence anampa Christine kitabu cha Lolita pamoja na ujumbe apeleke kwa Mr Brundish, anamuomba akisome na amshauri kama ni kitabu kizuri ambacho watu watakipenda.
Siku nyingi baadaye Mr Brundish anatuma ujumbe Florence aende kwake, anafika na anampongeza kwa ujasiri wa kufungua duka hilo, siyo wengi wanao.
Pia anamuuliza amejipangaje kukabiliana na Mrs Gamart, Florence anajibu hamhofii kwa chochote.
Mr Brundish anamwambia anafanya makosa, maana Mrs Gamart anajuana na watu wakubwa, lazima atamsumbua.
Florence anamwambia kilichomleta ni kutaka kujua kama kitabu alichomtumia ni kizuri na watu watakipenda. Anamjibu kwa maoni yake ni kizuri, japo watu wanaweza wasikielewe, watakinunua.
Florence anashukuru kwa hilo, Mr Brundish anamuuliza kwa nini amemuamini yeye kumpa maoni wakati wanawake huwa ni wazuri kwenye maoni kuliko wanaume? Florence anamjibu wanaume huwa hawajutii maamuzi yao kama wanawake.
Florence anaagiza nakala 25 za kitabu hicho cha Lolita, mzigo unapofika Christine anamshangaa na kumuuliza iweje ameagiza mzigo mkubwa hivyo wakati hawajawahi kuuza nakala nyingi kiasi hicho cha kitabu kimoja?
Wanapangilia vizuri kitabu hicho kipya ili wateja waweze kukiona.

👉8
Mwanasheria wa Florence anayeitwa Mr Thornton anamtumia barua kwamba amepokea malalamiko kutoka kwa mwanasheria wa Mrs Gamart kwamba duka la vitabu limekuwa linaleta usumbufu kwa wakazi wa mji huo.
Kwani wateja wamekuwa wanajazana eneo ambapo vitabu vinaoneshwa kiasi cha kuziba barabara.
Florence anamtaka mwanasheria huyo atembelee duka kisha kumshauri, anafanya hivyo na kumwambia kweli duka linaleta usumbufu hivyo anamshauri asiweke kitabu kipya eneo la maonesho na amuombe Mrs Gamart msamaha ili asimfungulie kesi
Florence anamjibu hatafanya hivyo. Na hilo linaishia hapo.
Kitabu kipya cha Lolita kinaleta mafanikio makubwa, kinawavutia wengi, mauzo yanakuwa makubwa na kinaongeza faida sana.
Tangu kuanza kuuza kitabu hicho kazi zimekuwa nyingi na Florence pamoja na Christine wamekuwa wanachoka sana.
Mkaguzi wa elimu anatembelea shule anayosoma Christine na kusema anaangalia kama wanafunzi walioajiriwa kwa kazi za muda wanapata muda wa kutosha kwenye masomo yao.
Anamchukua Christine na kumhoji kwa muda kisha kumwandikia Florence barua kwamba pamoja na Christine kuwa na mahudhurio mazuri shule, wamegundua tangu waanze kuuza kitabu kipya cha Lolita amefanya kazi masaa mengi wakati wa likizo, kitu ambacho siyo kizuri kiafya. Hivyo wanatumia sheria ya elimu kumkataza asiendelee kumtumia Christine kwenye kazi za ziada.
Florence anajibu sheria wanayotumia inahusu watoto wa kuanzia miaka 14 na kuendelea, Christine ana miaka 11 na anaruhusiwa kufanya kazi ndogo ndogo kwa muda wa ziada.
Hilo pia linaishia hapo, haliendelei.
Florence anapata taarifa kwamba mpwa wa Mrs Gamart ambaye ni mbunge ametoa pendekezo la sheria inayotaka majengo yote yenye miaka zaidi ya 500 na ambayo hayatumiki kwa makazi yanunuliwe na serikali za miji ili yatumike kama sehemu za watu kujifunza na kupumzika.
Florence anaona sheria hiyo haitamhusu yeye na jengo kuu, kwani licha ya kuwa na miaka zaidi ya 500 na kulitumia kwa biashara, amekuwa akiishi hapo pia, hivyo atalichukulia kama jengo la makazi.

👉9
Christine anafanya mtihani wa mwisho, matokeo yanatoka, hajapata ufaulu wa kuendelea na elimu ya juu, hivyo anaenda shule ya ufundi.
Hataweza tena kumsaidia Florence kwenye duka. Wanaagana na Florence anamuuliza kama akipata muda atakuwa anakuja, anamjibu hajui kama itawezekana.

Aliyekuwa anamsaidia Florence kukagua hesabu za biashara pia amepandishwa cheo kazini kwake, majukumu yamekuwa mengi hivyo hawezi tena kumsaidis.
Florence anajikuta na majukumu mengi yanayomlazimu kufanya kazi muda mrefu, kitu kinachomchosha sana.
Milo anamtembelea Florence na kumuona alivyochoka, anamwambia yuko tayari kumsaidia maana huwa anakuwa na muda jioni. Florence anamwambia kiasi alichokuwa anamlipa Christine na kwamba hawezi kulipa zaidi ya hapo. Milo anakubali kumsaidia.
Mependekezo ya sheria ya majengo ya zamami inapitishwa na bunge na inaonekana kuwa na mabadiliko ambayo yanafanya manunuzi hayo kuwa ya lazima na siyo hiari.
Mauzo kwenye duka la vitabu pia yamepungua sana, wateja ni wachache na wanaonunua ni wachache zaidi ukilinganisha na kipindi cha nyuma.

👉10
Mr Brundish anaonekana akitoka kwenye nyumba yake na kwenda kwenye nyumba ya Mrs Gamart.
Kila mtu anashangazwa na hilo maana kwa miaka mingi hajaonekaba nje ya nyumba yake.
Anafika kwa Mrs Gamart, hali yake ni dhoofu sana.
Anamwambia Mrs Gamart kilichomleta ni kumtaka aache kumsumbua Florence, amuache aendelee na biashara yake kwa sababu hajamsumbua yeyote.
Mrs Gamart anamjibu yeye hajamsumbua, bali sheria ndiyo inafuata mkondo wake. Mr Brundish anamwambia anajua vizuri sana kwamba sheria hiyo imetokana na yeye kutumia watu anaojuana nao kuitunga na kuipitisha.
Mr Brundish anamwambia anajua njia mbalimbali za kuizuia sheria hiyo isimuathiri Florence, hivyo anachotaka ni Mrs Gamart akae mbali naye na aache kumsumbua.
Anatoka kurudi kwake na akiwa njiani anaaguka na kufariki dunia.
Mazishi yake yanahudhuriwa na wengi kutoka miji mbalimbali, inaonekana alijulikana na wengi.
Florence anapokea notisi ya kuondoka kwenye jengo kulingana na sheria hiyo mpya.
Kutokana na hali ya uchakavu wa jengo, hatafidiwa fedha kwa jengo hilo. Hivyo anaambiwa aondoe vitabu vyake kwenye jengo hilo.
Anauliza mwanasheria wake ambaye anamjibu hawana cha kufanya kwa sheria hiyo mpya.
Meneja wa benki anamtaka Florence waonane kujadili mkopo aliochukua. Kwa kuwa jengo halifidiwi, anamtaka auze vitabu vyote alivyonavyo na gari yake pia ili kufidia mkopo.
Florence anajikuta hana nyumba, hana duka na hana gari. Anakata tiketi ya kuondoka kwenye mji huo.
Anaondoka akiwa ameinama kwa aibu kwa sababu mji alioishi kwa zaidi ya miaka 10 haujataka kuwa na duka la vitabu.

👉SOMO
Riwaya hii ina mengi ya kutufundisha kuhusu biashara na maisha kwa ujumla.
Tumejifunza uthubutu na ujasiri ambao Florence amekuwa nao katika kuanzisha biashara na kupambana ili ifanikiwe licha ya vikwazo mbalimbali alivyokutana navyo.
Tumejifunza pia mambo ya kuzingatia wakati unaanzisha biashara, kuanzia lengo, kuijua biashara vizuri na kujua hesabu wa fedha kwenye biashara.
Tumejifunza jinsi ambavyo baadhi ya watu hawapendi kuona wengine wakipoga hatua. Mrs Gamart amefanya kila mbinu kuhakikisha anaua biashara ya Florence, mbinu nyingi za awali zilishindwa mpaka alipoweza kulaghai mabadiliko ya sheria.
Tumeoja jinsi watu wanavyoweza kutuamini na kuwa tayari kutusaidia na hata kutupigania hata kama hilo linaweka maisha yao hatarini. Mr Brundish amekuwa msaada mkubwa kwa Florence, kuanzia kumtia moyo kwa kuanzisha duka la vitabu, kuwa tayari kumshauri kununua kitabu cha Lolita na hata kumkabili Mrs Gamart asimsumbue.
Mwisho kabisa tunajifunza siyo kila fursa unayoiona inaweza kuwa nzuri kwako. Unaweza kuona eneo fulani halina biashara fulani na ukaona hiyo ni fursa, kumbe eneo hilo halihitaji kabisa biashara hiyo na

litapambana na wewe mpaka ushindwe. Hicho ndicho alichojifunza Florence mwanzoni kwamba mji wa Hardborough haukuwa unahitaji duka la vitabu.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania